Rather than signalling a diplomatic shift away from longstanding partners, the visit reflects Tanzania's enduring commitment to independent, non-aligned and interest-driven diplomacy, an approach rooted in the country's post-independence history and increasingly relevant in a multipolar world.

At its core, President Samia's engagement with Russia appears less about geopolitical positioning and more about economic pragmatism. The discussions centred largely on trade, mining, energy, transport, agriculture, logistics and industrial cooperation, sectors that remain central to Tanzania's ambitions for economic transformation and regional competitiveness.

For a country seeking to industrialise, expand infrastructure and create jobs for a rapidly growing population, broadening international partnerships is not simply a diplomatic exercise; it is an economic necessity.

The visit also reflects a wider reality confronting many African nations today: development opportunities are no longer confined to traditional Western partnerships alone. Emerging economies, BRICS countries and Gulf states are increasingly becoming important sources of investment, technology, trade and infrastructure financing.

In that context, Tanzania's outreach to Russia can be seen as part of a broader strategy aimed at diversifying economic relationships while preserving the country's strategic autonomy.

Far from abandoning existing alliances, the approach suggests a presidency seeking to navigate a changing global landscape with flexibility, balance and a clear focus on national development priorities.

For decades, Tanzania has pursued a foreign policy grounded in sovereign decision-making, strategic independence and constructive engagement with nations

across the world, regardless of ideological or geopolitical differences.

Closely associated with the vision of the country's founding father, Mwalimu Julius Nyerere, this approach was never intended to isolate Tanzania from global powers or align it permanently with any particular bloc. Instead, it sought to preserve the country's freedom to engage internationally on the basis of national interest, mutual respect and shared development goals.

That philosophy remains highly relevant in today's changing global landscape.

The international economy is becoming increasingly multipolar, with emerging economies, BRICS countries, Gulf States and Asian powers playing a growing role in shaping global trade, finance, technology and energy systems. In such an environment, developing countries like Tanzania are increasingly seeking diversified partnerships capable of supporting economic transformation, industrial growth and long-term resilience.

The issue facing Tanzania, therefore, is not whether it should cooperate with the West or with countries such as Russia, China or India. Rather, it is how the country can engage constructively with all major centres of global economic influence while safeguarding its sovereignty and advancing its national development priorities.

This broader outlook appears central to President Samia Suluhu Hassan's approach to diplomacy.

Some critics of the Russia visit have pointed to the relatively modest trade volumes

between Tanzania and Russia compared to Western economies. While those figures may be accurate, they do not fully capture how international economic partnerships are built and expanded over time.

Trade and investment relationships rarely emerge overnight. In most cases, they develop gradually through sustained political engagement, strategic dialogue, investor confidence and long-term cooperation frameworks.

Many of Tanzania's strongest international partnerships today were themselves shaped through years of diplomatic engagement, state visits and continued economic cooperation.

Viewed from that perspective, President Samia's visit to Russia reflects an effort to open new economic opportunities, deepen strategic cooperation and broaden Tanzania's global partnerships in line with the country's wider economic diplomacy agenda.

President Samia's visit to Russia should therefore be viewed not only through the lens of current trade figures, but also in terms of the broader economic opportunities it seeks to unlock for Tanzania in the years ahead.

Among the most significant areas of potential cooperation is the mining sector. Tanzania is endowed with strategic minerals such as graphite, nickel, uranium and rare earth elements resources that are increasingly critical to the global shift towards clean energy, electric vehicles, battery storage technologies and advanced manufacturing industries.

As demand for these minerals continues to rise

globally, Tanzania is seeking not only to expand extraction activities but also to strengthen local processing, value addition and industrial capacity. Russia's longstanding experience in geological exploration, mining technologies, mineral processing and nuclear energy development could provide valuable technical cooperation capable of supporting these ambitions.

The discussions surrounding uranium development are particularly significant. With many countries reconsidering nuclear energy as part of long-term clean energy strategies, uranium is regaining importance within the global energy transition.

Tanzania's uranium reserves therefore represent not only a commercial opportunity, but also a strategic national asset with the potential to contribute to future industrial growth and export earnings.

Cooperation in agriculture and fertiliser production could also carry substantial

“
Rather than signalling a diplomatic shift away from longstanding partners, the visit reflects Tanzania's enduring commitment to independent, non-aligned and interest-driven diplomacy, an approach rooted in the country's post-independence history and increasingly relevant in a multipolar world.
”



President Samia Suluhu Hassan and Russian Federation President Vladimir Putin take notes during the St Petersburg International Economic Forum (SPIEF '26) at the Expo Forum Convention Centre on the outskirts of St Petersburg in Russia, on Friday. (Photo by State House)

Equally, expanding maritime links between Russian ports and Dar es Salaam could reinforce Tanzania's growing role as a regional logistics and trade hub serving East and Central Africa. As the country continues investing in ports, railways and transport corridors, diversified international trade partnerships are becoming increasingly important to Tanzania's broader economic transformation agenda.

Tourism is another sector with considerable growth potential. Tanzania continues to attract increasing numbers of international visitors drawn by its globally renowned wildlife, pristine beaches, rich cultural heritage and world-class tourist destinations such as Serengeti, Kilimanjaro and Zanzibar.

Expanding engagement with Russia could help diversify tourism markets, strengthen people-to-people exchanges and broaden Tanzania's reach within emerging travel markets at a time when the country is seeking to grow its tourism industry further.

Beyond the economic dimension, the visit also carries important diplomatic significance.

For decades, Tanzania has earned international respect for its balanced, independent and principled diplomacy, rooted in peaceful engagement, mutual respect and constructive cooperation with nations across the world.

President Samia Suluhu Hassan's engagement with Russia reflects that enduring foreign policy tradition one that places dialogue, partnership and national development at the centre of interna-

tional relations.

At the same time, Tanzania continues to maintain strong and productive relations with the United States, the European Union and other longstanding international partners in areas such as health, education, infrastructure, trade and development cooperation. These partnerships remain important and continue to make valuable contributions to Tanzania's economic growth and social progress.

Viewed within this broader context, Tanzania's engagement with Russia should not be interpreted as a shift away from existing partners, but rather as part of a wider strategy aimed at expanding international cooperation, diversifying economic opportunities and strengthening the country's strategic position in an evolving global economy.

In today's evolving global landscape, diplomacy is increasingly defined by cooperation across multiple regions and economic blocs rather than rigid or exclusive alignments.

Countries across Africa, Asia and the Middle East are expanding partnerships with different global powers simultaneously in order to attract investment, strengthen economic resilience and advance their national development priorities.

India, for example, maintains close relations with both Russia and the United States, while Gulf nations continue deepening cooperation with China alongside longstanding partnerships with Western economies. Across Africa, governments are similarly pursuing diversified trade and investment relationships as

part of broader efforts to reduce economic vulnerability and create new growth opportunities.

Tanzania is pursuing that same pragmatic and forward-looking approach.

Within this context, President Samia Suluhu Hassan's recent visit to Russia should be viewed as part of Tanzania's wider economic diplomacy agenda, one aimed at expanding strategic partnerships, attracting investment and accelerating socio-economic transformation.

The visit created opportunities for deeper cooperation in key sectors including mining, energy, transport, agriculture, logistics, tourism and industrial development, all of which remain central to Tanzania's long-term growth ambitions.

Discussions surrounding strategic minerals, fertiliser production, transport connectivity and industrial cooperation carry significant potential for job creation, technology transfer, value addition and expanded trade.

Equally important, the engagements reinforced Tanzania's longstanding commitment to constructive international cooperation and mutually beneficial partnerships with countries across the world.

For decades, Tanzania has maintained a foreign policy grounded in independence, mutual respect and non-alignment while continuing to engage positively with both traditional and emerging global partners in pursuit of national development goals.

The country continues to enjoy strong relations with the United States, European nations, China, India, Gulf countries and other international partners, reflecting its enduring belief in cooperation based on sovereign equality and shared interests.

In an increasingly competitive global economy, strategic diversification of partnerships has become essential for developing nations seeking investment, technology, industrial growth and access to new markets.

President Samia's engagement with Russia reflects that broader reality.

Ultimately, the significance of the visit will be judged by the practical benefits it delivers to Tanzanians, including increased investment, expanded economic opportunities, stronger infrastructure, industrial growth and employment creation.

If the partnerships initiated during the visit translate into tangible economic gains and deeper development cooperation, the engagement will likely stand as another important step in Tanzania's ongoing efforts to strengthen its economy, expand its global partnerships and uphold its long-standing foreign policy principle of friendship with all and alignment to none.

Samia aamika 'mano' ziara ya Urusi

РОССИЯ - ТАНЗАНИЯ

RUSSIA - TANZANIA

forum-spb.ru



RAIS Samia Suluhu Hassan ameeleza manufaa ambayo Tanzania 'itavuna' kutokana na ziara yake nchini Urusi aliyohitimisha juzi kabla ya kurejea nchini jana.

Akizungumza katika mahojiano na waandishi wa habari kuhusu ziara hiyo, alisema ni mwanzo wa ushirikiano utakaosaidia kukuza biashara na kuzalisha ajira kwa vijana nchini.

Aidha, amesema Tanzania inaelekea katika uzalishaji wa umeme wa nyuklia kwa kushirikiana na Urusi.

Ajira vijana

Alisema asilimia 60 ya idadi ya Watanzania ni vijana, hivyo mambo mengi waliyozungumza katika ziara hiyo ni kwa ajili ya kundi hilo nchini.

Alisema ipo fursa kubwa kwenye kilimo na tayari wameingia kwenye kilimo cha uzalishaji wa ndizi ambazo zina soko kubwa Urusi.

"Warusi tumewapa kama hekta 6,000 kule Morogoro na wanaangalia nyingine ili wapande ndizi. Vijana wetu watakata ajira na kutakuwa na biashara kubwa," alisema.

Alisema ajira nyingine zitatokana na uwekezaji wa viwanda, kwenye kuongeza thamani ya mazao ya kilimo

na viwanda vitakavyozalisha dawa, chanjo kwa ajili ya watu na Wanyama. "Ajira ni kwa watoto wetu," alisema Rais Samia.

Ajira mradi urani

Pia, alisema mradi wa urani wa Mkuju utaajiri vijana 20,000 katika fani mbalimbali na ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Tanzania nchini Urusi unatarajiwa kuongezeka.

"Tunapata ufadhili nafasi 150 kwa mwaka lakini tumeomba katika mazungumzo yetu na Rais Putin (Vladimir) ametukubalia atatuongeze nafasi zaidi, watakaokuja kusoma hapa ni vijana wa Tanzania," alisema.

Alisema, "kati yao kuna wanaosomesha na Serikali ya Urusi na wengine ambao wapo kwenye masomo ya sayansi ya nyuklia wanalipwa na Kampuni ya Mantra au Rosatom na serikali inajazia."

Alisisitiza, "Biashara za vijana, tumesema tuna fedha kwa ajili ya vijana, ATCL inaanza safari kuja Urusi. Hii ndege itajaa, kuja itajaa kurudi, itaenda na watalii itarudi na watalii, itaenda na wafanyabiashara itarudi nao, ni vijana wa Kitanzania watakaofanya hiyo biashara."

Kwa mujibu wa Rais Samia, mazungumzo yaliyofanyika baina ya jumuiya

ya wafanyabiashara wa Tanzania na Urusi, sehemu kubwa ya mambo watakayokubaliana ni vijana wa Tanzania watakaofanya biashara, watakaopata ajira

katika biashara.

Alisema Tanzania ni kati ya nchi tatu Afrika zenye uwapo mkubwa wa urani ambayo hutoa nishati ya nyukliana huzalisha bidhaa

nyingi ukiwemo umeme.

Alisema kwamba wameingia mkataba na Kampuni ya Rosatom ambayo imefanya majaribio ya awali ya kuchimba urani.

“Wanasema teknolojia waliyotumia kwenye majaribio imeleta faida lakini haikufikia ufanisi; wamepungukiwa kwa asilimia 25, walichofanya wameongeza teknolojia ili wafidie upungufu wa asilimia 25 wapate matokeo makubwa zaidi, watakapokuwa wanazalisha hiyo uranium kuna uranium ambayo wataichukua wataendeleza, madini mengine watasafirisha kwa matumizi yao huku mengine watazalishia umeme,” aliongeza.

Umeme nyuklia

Alisema, mazungumzo yote wanayofanya na wawekezaji hao yanapaswa kufuata masharti ya Wakala wa Kimataifa wa Nishati ya Atomiki na watakapokubaliana ndipo yafanyike mazungumzo ya kuingia mikataba.

“Wao wanasema ikifika 2029 kinu cha mwanzo cha uzalishaji wa umeme wa nyuklia kitakuwa tayari, kwa hiyo tunakwenda huko lakini tuna kazi kubwa ya kuwafundisha Watanzania kuwaeleza kwamba umeme huu hauna hatari, ni umeme

kama mwingine na unakwenda kutuongezea umeme wetu na kufanya Tanzania kuwa kituo kikubwa cha biashara," alisema.

Nchi kutofungamana

Aidha, alisema Tanzania inafuata kanuni ya kutofungamana na upande wowote na kwamba kila anayetaka kufanya kazi nayo itafanya naye kazi.

Alisema pia katika suala la diplomasia ya uchumi, kila inapokuja fursa ya kukuza uchumi fursa hiyo itatumika.

"Tunaposema kutofungamana na upande wowote, pamoja na kwamba Urusi muda mrefu hapa hapakuwa na mambo yanayoendelea kutokana na sababu kadhaa, lakini tumekuwa tukifanya kazi na wengine," alifafanua.

Ziara ya kihistoria

Alisema Urusi ni mshirika mkubwa wa Tanzania tangu miaka ya 1960. Alisema tangu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alipofanya ziara 1969 nchini humo, hakuna kiongozi mwingine mkubwa wa nchi ambaye amefanya isipokuwa yeye ikiwa ni baada ya miaka 57.

Aliongeza kuwa lengo la ziara ya Urusi ni kuwahakikishia kwamba Tanzania bado inawahitaji na ina mengi ya kufanya nao kwa maendeleo yao na nchini.

"Kuwahakikishia kwamba Tanzania tumefungua milango na unapofungua milango wa kwanza kumshika mkono mwende pamoja kwenye maendeleo ni ndugu yako, huyu ni ndugu yetu ambaye alitushika mkono siku nyingi pamoja na wengine," alisema.

Aliendelea, "Kwa hiyo tumekuja kuwahakikishia kwamba Tanzania tupo pamoja nao tumefungua milango, tuna maeneo kadhaa ya ushirikiano waje tufanye kazi pamoja".

Dira 2050

Alisema katika ziara yake wameenda na maombi maalumu ambayo yote yamepokewa.

Rais Samia alisema waliwakuta wamesoma Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 na wameibua maeneo tisa na Tanzania ilienda na mambo manane ambayo wamejadili kuanza kuyafanyia kazi.

Aliongeza kuwa miradi wanayopanga kutekeleza inaibuliwa kutokana na vipaumbele vya kwenye dira hiyo.

Ziara ya Rais Samia Urusi yaonesha Diplomasia Huru na Dira ya Maendeleo

Na Mwandishi Wetu

ZIARA ya hivi karibuni ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Urusi imezua mjadala mpana ndani na nje ya Tanzania, huku baadhi ya wakosoaji wakihoji umuhimu wa kimkakati wa kuimarisha ushirikiano na Urusi wakati ambao dunia inakabiliwa na mvutano mkubwa wa kisiasa na kijeshi.

Mijadala ya aina hii si jambo la kushangaza wala si baya. Uamuzi wa sera za kigeni, hasa yale yanayohusisha mataifa makubwa duniani, mara nyingi huvutia tafsiri tofauti zinazotokana na mitazamo ya kisiasa, kiuchumi na kiitikadi.

Hata hivyo, kuichukulia ziara hiyo kama hatari ya kisiasa pekee kunapuuza muktadha mpana wa utamaduni wa sera ya mambo ya nje ya Tanzania pamoja na hali halisi ya uchumi wa kimataifa wa sasa.

Badala ya kuashiria mabadiliko ya kidiplomasia yanayoitenga Tanzania na washirika wake wa muda mrefu, ziara hiyo inaonesha dhamira ya kudumu ya Tanzania ya kuendesha diplomasia huru, isiyo-fungamana na upande wowote na inayozingatia maslahi ya taifa.

Huu ni mtazamo uliojengwa tangu baada ya uhuru wa nchi na ambao unaendelea kuwa muhimu katika dunia yenye nguvu nyingi za kiuchumi na kisiasa.

Kwa msingi wake, ushiriki wa Rais Samia na Urusi unaonekana kuwa zaidi kuhusu programu ya kiuchumi kuliko kujipanga kisiasa katika kambi fulani za kimataifa.


Mazungumzo yalijikita katika biashara, madini, nishati, usafirishaji, kilimo, vifaa vya usafirishaji na ushirikiano wa viwanda, sekta ambazo ni muhimu kwa malengo ya Tanzania ya kubadilisha uchumi wake na kuongeza ushindani wa kikanda.

Kwa taifa linalolenga kuendeleza viwanda, kupanua miundombinu na kutengeneza ajira kwa idadi ya watu inayooongezeka kwa kasi, kupanua ushirikiano wa kimataifa si suala la diplomasia pekee, bali ni hitaji la kiuchumi.

Ziara hiyo pia inaakisi hali inayozikabili nchi nyingi za Afrika leo: fursa za maendeleo hazipatikani tena kupitia ushirikiano wa jadi na mataifa ya Magharibi pekee. Uchumi unaochipukia, nchi za BRICS na mataifa ya Ghuba yanazidi kuwa vyanzo muhimu vya uwekezaji, teknolojia, biashara na ufadhili wa miundombinu.

Katika muktadha huo, hatua ya Tanzania kuimarisha uhusiano na Urusi inaweza kuonekana kama sehemu ya mkakati mpana wa kupanua uhusiano wa kiuchumi huku ikidumisha uhuru wake wa kimkakati.

Badala ya kuacha ushirikiano uliopo, mbinu hii inaonesha uongozi unaotafuta kuendesha diplomasia kwa usawa, kubadilika kulingana na mazingira ya dunia yanayobadilika na kuweka mbele vipaumbele vya maendeleo ya taifa.



Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Shirikisho la Urusi, Vladimir Putin wakifuatilia Kongamano la Kimataifa la Uchumi la St. Petersburg (SPIEF'26) lililofanyika kwenye Ukumbi wa Kituo cha Mikutano cha ExpoForum nje ya Jiji la St. Petersburg nchini Urusi juzi. (Picha na Ikulu).

Kwa miongo kadhaa, Tanzania imeendesha sera ya mambo ya nje inayojengwa juu ya uhuru wa kufanya maamuzi, kujitegemea kimkakati na kushirikiana kwa njia chanya na mataifa mbalimbali duniani bila kujali tofauti za kiitikadi au kisiasa.

Mtazamo huu, unaohusishwa kwa karibu na maono ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, haukulenga kuitenga Tanzania na mataifa makubwa au kuifungamani-sha na kambi yoyote maalumu.

Badala yake, ulikuwa na lengo la kuhifadhi uhuru wa taifa kushirikiana kimataifa kwa kuzingatia maslahi ya taifa, heshima ya pande zote na malengo ya pamoja ya maendeleo.

Falsafa hiyo inaendelea kuwa muhimu katika mazingira ya sasa ya dunia.

Uchumi wa kimataifa unazidi kuwa wa pande nyingi, huku mataifa yanayoibukia, nchi za BRICS, mataifa ya Ghuba na nchi za Asia zikichukua nafasi kubwa zaidi katika biashara, fedha, teknolojia na mifumo ya nishati duniani.

Katika mazingira hayo, nchi zinazoendelea kama Tanzania zina- tafuta ushirikiano mpana unaoweza kusaidia mageuzi ya kiuchumi, ukuaji wa viwanda na uimara wa muda mrefu.

Kwa hiyo, kwa Tanzania si kama inapaswa kushirikiana na nchi za Magharibi au na mataifa kama Urusi, China na India. Badala yake, ni jinsi gani inaweza kushirikiana kwa njia yenye manufaa na vituo vyote vikuu vya nguvu za kiuchumi duniani huku ikilinda uhuru wake na kusukuma mbele ajenda yake ya maendeleo.

Mtazamo huo mpana unaonekana kuwa sehemu muhimu ya diplomasia ya Rais Samia.

Baadhi ya wakosoaji wa ziara ya Urusi wameelekeza kwenye kiwango kidogo cha biashara kati ya Tanzania na Urusi ikilinganishwa na

mataifa ya Magharibi.

Ingawa takwimu hizo zinaweza kuwa sahihi, hazioneshi kikamilifu namna uhusiano wa biashara na uwekezaji unavyojengwa na kukua kwa muda.

Uhusiano wa biashara na uwekezaji mara chache huibuka ghafla. Mara nyingi hujengwa hatua kwa hatua kupitia mawasiliano ya kisiasa ya kudumu, mazungumzo ya kimkakati, kuaminika kwa mazingira ya uwekezaji na mifumo ya ushirikiano wa muda mrefu.

Ushirikiano mwingi imara ambao Tanzania inao leo ulijengwa kupitia miaka ya ushirikiano wa kidiplomasia, ziara za viongozi na ushirikiano wa kiuchumi unaoendelea. Kwa mtazamo huo, ziara ya Rais Samia nchini Urusi inaonesha jitihada za kufungua fursa mpya za kiuchumi, kuimarisha ushirikiano wa kimkakati na kupanua mahusiano ya Tanzania duniani kwa mujibu wa ajenda yake ya diplomasia ya uchumi.

Ziara hiyo inapaswa kutazamwa si kwa kuzingatia tu kiwango cha sasa cha biashara, bali pia kwa kuangalia fursa pana za kiuchumi ambazo inaweza kufungua kwa Tanzania katika miaka ijayo.

Mojawapo ya maeneo muhimu ya ushirikiano ni sekta ya madini. Tanzania imejaliwa kuwa na madini ya kimkakati kama grafiti, nikeli, urani na madini adimu ya ardhini ambayo ni muhimu katika mpito wa dunia kuelekea nishati safi, magari ya umeme, teknolojia za kuhifadhi nishati na viwanda vya kisasa.

Kadiri mahitaji ya madini hayo yanavyoongezeka duniani, Tanzania inalenga si tu kuongeza uchimbaji wake, bali pia kuimarisha uchakataji wa ndani, kuongeza thamani na kukuza uwezo wa viwanda.

Uzoefu wa Urusi katika utafiti wa jiolojia, teknolojia za madini, uchakataji wa madini na maendeleo ya nishati ya nyuklia unaweza ku-

saidia kufanikisha malengo hayo.

Mazungumzo kuhusu maendeleo ya sekta ya urani yana umuhimu wa pekee. Wakati mataifa mengi yanapozingatia tena nishati ya nyuklia kama sehemu ya mikakati ya muda mrefu ya nishati safi, urani inazidi kupata umuhimu katika mabadiliko ya mfumo wa nishati duniani.

Ushirikiano katika kilimo na uzalishaji wa mbolea pia unaweza kuleta manufaa makubwa ya muda mrefu.

Matatizo ya hivi karibuni katika minyororo ya usambazaji duniani yalionesha udhaifu wa nchi nyingi zinazoendelea kutokana na kupanda kwa bei za mbolea na kutokuwa na uhakika wa masoko ya pembejeo za kilimo.

Kuimarisha ushirikiano na uzalishaji wakubwa wa mbolea kama Urusi kunaweza kusaidia kuongeza tija ya kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kupunguza athari za mishtuko ya usambazaji katika siku zijazo.

Usafirishaji na huduma za vifaa vya usafiri pia zilikuwa maeneo muhimu ya mazungumzo.

Kuanzishwa kwa safari za moja kwa moja za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kati ya Dar es Salaam, Moscow na Zanzibar ni zaidi ya hatua ya kidiplomasia ya mfano. Muunganisho bora wa anga unaweza kuchochea utalii, kurahisisha safari za biashara, kuimarisha usafirishaji wa mizigo na kuongeza biashara kati ya Afrika Mashariki na masoko ya Eurasia.

Vilevile, kuimarisha usafiri wa baharini kati ya bandari za Urusi na Dar es Salaam kunaweza kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu cha biashara na usafirishaji kwa Afrika Mashariki na Kati.

Wakati nchi inaendelea kuwekeza katika bandari, reli na korido za usafiri, ushirikiano mpana wa biashara unakuwa muhimu zaidi kwa mageuzi yake ya kiuchumi.

Utalii ni sekta nyingine yenye uwezo mkubwa wa ukuaji. Tanzania inaendelea kuvutia watalii wengi kutoka duniani kote kutokana na wanyamapori wake maarufu, fukwe safi, urithi wa kitamaduni na vivutio vya kimataifa kama Serengeti, Kilimanjaro na Zanzibar.

Mbali na masuala ya kiuchumi, ziara hiyo pia ina umuhimu mkubwa wa kidiplomasia.

Kwa miongo kadhaa, Tanzania imeheshimiwa kimataifa kwa diplomasia yake ya usawa, uhuru na misingi ya kuheshimiana, mazungumzo ya amani na ushirikiano wa kujenga.

Ushirikiano wa Rais Samia na Urusi unaendeleza utamaduni huo wa muda mrefu wa sera ya mambo ya nje unaoweza mazungumzo, ushirikiano na maendeleo ya taifa katika kiini cha mahusiano ya kimataifa.

Wakati huohuo, Tanzania inaendelea kuwa na mahusiano imara na yenye tija na Marekani, Umoja wa Ulaya na washirika wengine wa muda mrefu katika sekta za afya, elimu, miundombinu, biashara na maendeleo. Ushirikiano huu unaendelea kuwa muhimu kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii nchini.

Kwa mtazamo huu mpana, ushirikiano wa Tanzania na Urusi haupaswi kutafsiriwa kama kuachana na washirika waliopo, bali kama sehemu ya mkakati wa kupanua ushirikiano wa kimataifa, kuongeza fursa za kiuchumi na kuimarisha nafasi ya taifa katika uchumi wa dunia unaobadilika.

Katika mazingira ya sasa ya dunia, diplomasia inazidi kutawaliwa na ushirikiano na maeneo mbalimbali ya dunia badala ya kufungamana na upande mmoja pekee.

Mataifa ya Afrika, Asia na Mashariki ya Kati yanapanua uhusiano wao na nguvu mbalimbali za dunia kwa wakati mmoja ili kuvutia uwekezaji, kuimarisha uchumi na kufanikisha malengo yao ya maendeleo.

Kwa mfano, India ina uhusiano mzuri na Urusi pamoja na Marekani, huku mataifa ya Ghuba yakiendelea kuimarisha ushirikiano na China sambamba na ushirikiano wao wa muda mrefu na nchi za Magharibi. Afrika pia inashuhudia serikali nyingi zikipanua mahusiano ya biashara na uwekezaji ili kupunguza utegemezi wa upande mmoja na kuunda fursa mpya za ukuaji.

Tanzania nayo inafuata mkondo huo wa kimkakati na wa kuangalia mbele. Muhimu pia, mazungumzo hayo yameimarisha dhamira ya Tanzania ya kuendelea kushirikiana kwa njia yenye manufaa na mataifa mbalimbali duniani.

Kwa miongo kadhaa, Tanzania imeendelea kuendesha sera ya mambo ya nje inayojengwa juu ya uhuru, kuheshimiana na kutofungamana na upande wowote huku ikishirikiana kwa karibu na washirika wa jadi na wale wanaoibukia kwa ajili ya maendeleo ya taifa.